**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Tano – Tarehe 11 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

63. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kukabiliana na changamoto ya makaazi ya Viongozi Wakuu wa Serikali huko Pemba, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilijenga jengo jipya huko Pagali Pemba ambalo limeshaanza kutumiwa. Hata hivyo, katika eneo la jengo hilo hakukuwekwa taa ambazo zingeimarisha haiba na ulinzi wa eneo hilo.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haikuweka taa katika eneo hilo.

(b) Je, ni gharama ya kiasi gani zilizotumika katika ujenzi wa jengo hilo jipya pamoja na ujenzi wa barabara kutoka Gombani hadi Tibirinzi.

**<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:</u>**

148. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Maadiliko ya Tabia ya Nchi yamesababisha maeneo mbali mbali ya kilimo kuvamiwa na maji chumvi kutoka baharini na hatimaye maeneo hayo hupoteza sifa katika masuala ya kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu.

(a) Je ni hatua gani zilizochukuliwa na Serikali kupambana na tatizo hili sugu.

(b) Je, ni utaratibu gani uliochukuliwa na Serikali wa kuwapatia kazi mbadala wakulima ambao wamejikita katika shughuli za kilimo ambao maeneo yao yamevamiwa na maji chumvi.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

84. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na juhudi kubwa za kuimarisha huduma za afya katika Kituo cha Afya Ukunjwi, ambapo hivi sasa huduma za uzalishaji zinapatikana na kuwarahisishia wakaazi wa vijiji vya jirani kupata huduma hizo kwa ukaribu zaidi, licha ya kuwepo kwa changamoto ya madaktari na majengo inayorudisha nyuma huduma za afya katika kituo hiki.

(a) Je, Serikali imepanga kuchukua hatua gani za haraka kukabiliana na changamoto ya madaktari katika kituo hiki ambacho kina daktari mmoja tu kwa huduma zote zinazotolewa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo jipya ambalo litakidhi mahitaji ya huduma za afya katika kituo hiki.

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuwepo kwa changamoto hizi ni kuhatarisha afya na maisha ya wakaazi wa Ukunjwi na vitongoji vyake.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

98. MHESHIMIWA MWANAASAHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Eneo la Fumba limebahatika kuwa sehemu ya uwekezaji hapa nchini. Hata hivyo, kuna changamoto katika uwekezaji huo kwa wananchi ikiwemo mipaka ya maeneo ya matumizi ya ardhi kwa wawekezaji pamoja na wananchi wa eneo la Fumba.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kubainisha kwa uwazi na kuwaeleza wananchi mipaka halisi ya eneo la uwekezaji na maeneo ya matumizi kwa ajili ya wananchi.

(b) Kutobainishwa kwa mipaka hiyo ya maeneo ya uwekezaji na yale ya matumizi ya wananchi, Je, Serikali haioni kuwa kunaweza kupelekea migogoro ya ardhi isiyokuwa ya lazima.

(c) Wananchi wa Fumba wategemee lini utafanyika mpango huo wa kubainisha kwa uwazi mipaka hiyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

6. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana ya ujenzi wa barabara ya Mpendae inayotoka Kwa Mchina hadi skuli ya Jang’ombe ambayo hata aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mpendae Marehemu Salim Abdalla Turkey aliwahi kutoa fedha taslim shilingi milioni 100 ili kusaidia ujenzi huo.

(a) Je, Serikali inalifahamu kwa kiasi gani suala hili.

(b) Ni sababu gani za msingi na za kitaalamu zilizosababisha kukwama kwa ujenzi wa barabra hiyo.

(c) Je, Serikali inatoai ahadi gani ya kuijenga barabara hiyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

86. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR HASSAN (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Inaonekana soko la kununua karafuu Zanzibar limeshuka kwani kuna karafuu ambazo zimechumwa tokea kipindi kilichopita na bado hazijauzwa, hali inayosababishwa na uhaba wa fedha wa Shirika la ZSTC.

(a) Je, ni lini soko la karafuu litakuwa tayari ili wananchi wauze karafuu zao kabla ya msimu mwengine kuanza.

(b) Kama soko limeshuka, Je, Wizara inawaahidi nini wananchi waliochuma karafuu kwa gharama katika awamu iliyopita.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais**,** Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**11 Mei, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**